# The Apostolic Life Community of Priests in the Opus Spiritus Sancti.

Africa Province.

E-Mail: alcp.africaprovince@yahoo.com

Office Mobile: +255 715 429 516

Provincialate Office
P. O. Box 734,
Moshi – Tanzania.

10th December, 2023

**Waraka/Majilio-Noeli, 2023**

Wapendwa Mapadre na Mashemasi, ALCP/OSS,

Salaam toka Makao ya Shirika-Kanda na Nyumba MAMA, Sabuko-Sanya Juu, Tanzania.

1. **Kuzinduliwa kwa Mwaka wa Jubilee ya uwepo wa Shirika, ALCP/OSS, miaka-50-**

   Tunamshukuru Mungu kwamba tarehe 21.11.2023 tumeadhimisha vema ibada ya uzinduzi wa Jubilee ya dhahabu (miaka-50-) ya uwepo wa Shirika letu la Mapadre wa Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu (ALCP/OSS).

   - Baba Askofu alituwashia Mshumaa wa Jubilee.
   - Sala ya Jubilee ilisaliwa >Hii isaliwe muda wote wa mwaka wa Jubilee.
   - Baba Askofu alizindua Kitabu cha Historia ya Shirika, Kanda ya Afrika. Ni Kitabu cha kusoma na kuwa na uelewa wa historia ya Shirika.
   - Mapadre wote tumekabidhiwa UPYA MSALABA WA SHIRIKA WA UTUME. Popote tunapotumwa uwe na msalaba huo wenye ALAMA maalum kwetu Kishirika na Kikanisa kwenye utume wetu. Msalaba huo utunzwe na utoe cheche za kutukumbusha daima utume wetu kama Mapadre wa Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu (ALCP/OSS).
     **Mapadre ambao hawakuwepo kwenye ibada ya uzinduzi ambapo kila Padre alikabidhiwa upya msalaba huo wa utume, basi wafike Shirikani na wapatiwe.**
   - Mkuu wa Shirika Kimataifa (Superior General) alitangaza rasmi kwenye ibada hii kuzinduliwa kwa mwaka wa Jubilee ya dhahabu ya Shirika la Mapadre wa Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu (ALCP/OSS). Kwa tangazo hilo rasmi, basi hili kwetu linakuwa siyo tu ni adhimisho la Shirika bali pia na zaidi ni adhimisho la Kanisa. Tukazane basi kuwa vyombo bora zaidi kwa Shirika na Kanisa kwenye utume wetu. Na Baba Askofu akatangaza **KAULI MBIU** kuwa ni **MSIKILIZE ROHO MTAKATIFU, KILA WAKATI** kwa Kiingereza ni; **LISTEN TO THE HOLY SPIRIT, ALL THE TIME.**
   - Imepandishwa kwenye mlingoti bendera ya Jubilee (Ina NEMBO ya Jubilee) kama ilivyotumwa kwenu. Bendera hii itapepea muda wote wa Mwaka wa Jubilee hadi kilele chake tarehe 21.11.2024. Sambamba na bendera hii zitapepea bendera za Mataifa yafuatayo yenye historia ya karibu sana na Shirika. Haya ni> Tanzania, Vatican, Ujerumani na India (kisha bendera ya Jubilee lilivyosemwa juu).

Bendera hizi zitapepea palipo na Makao Makuu ya Shirika kiulimwengu huko Soweto, Moshi/Tanzania, palipo na Makao Makuu ya Shirika-Kanda ya Afrika Sabuko, Sanya Juu/Tanzania na palipo Makao Makuu ya Shirika-Kanda ya India huko Hyderabad/India. Senta ni hizo tatu rasmi za kupepea bendera hizo kwa mwaka wote wa Jubilee. Kwingineko wanaweza pia bali siyo rasmi (Senta nyingine za Shirika).

- Baba askofu alituasa kwenye ibada takatifu kwamba wakati huu wa mwaka wa Jubilee, mambo manne yafanyiwe kazi;
  - Roho ya **SALA** itawale katika kipindi chote cha Mwaka wa Jubilee. Wanashirika tusali kwa bidii Zaidi.
  - Kuwepo na roho ya kufanya **TOBA.** Yawepo matendo ya toba na kupenda kufanya toba.
  - Roho ya **UPATANISHO** ionekane. Wanashirika tupende kupatana; kujipatanisha na wengine na Mungu.
  - **KARAMA** ya Shirika ifufuke na kudhihirika kwa maisha na vitendo.

## 2. Maadhimisho mengine

- Jubilee ya miaka 25 ya Upadre >Angalia utaratibu chini.
- Mafungo ya mwaka 2024 na semina >Anagalia chini. Tuma Jina lako unahudhuria Kundi lipi.
- Kutumwa kwa Mapadre wapya >ni Jumatatu tarehe 29.01.2024 Sabuko. Misa ya Roho Mtakatifu.

## 3. Mkutano Mkuu wa Shirika-Kanda (Provincial chapter), Novemba, 2024

Kadiri ya taratibu ya Shirika, Mkutano Mkuu wa Kanda huwepo kila baada ya miaka mitatu. Hivi, kwa mpango huo, Mkutano Mkuu wa Kanda unapaswa kuwepo Novemba, 2024. Muda huu pia yapo maadhimisho ya Mwaka wa Jubilee ambayo kilele chake ni tarehe 21 Novemba, 2024. **IWEJE? Mkutano Mkuu wa Kanda utakuwepo mara baada ya maadhimisho ya kilele cha Jubilee ya Shirika. Utaratibu wenyewe utatolewa mapema kuweza kujiandaa kwa wajumbe wa Mkutano na Jubilee.**

## 4. Utume

- Fr. JohnBosco Msafiri > Utume Ujerumani Jimbo la Regensburg.
- Fr. Innocent Mkwe > Utume Ujerumani Jimbo la Regensburg.
- Fr. Samuel Pancras Hamaro >Utume Mafinga kwenye mradi wa shamba.
- Fr. Alex Silvest >Toka Parokia ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu, Kakonko-Kigoma na kwenda Parokia ya Wat. Petro na Paulo, Mitume-Gairo-Morogoro kama Wakili Paroko.
- Fr. James Kichwa Riziki >Kutoka Parokia ya Wat. Petro na Paulo, Mitume, Gairo-Morogoro na kwenda Parokia ya Mt. Paulo mwongofu, Ngarenairobi-Moshi kama Paroko.

- Fr. Gilbert Kiusa >Kutoka Parokia ya Mt. Paulo mwongofu, Ngarenairobi-Moshi na kwenda Parokia ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu, Kakonko-Kigoma kama Wakili Paroko.
- Fr. Antipas K. Joseph >Kutoka Uaskofuni Moshi na kwenda Roma kwa masomo (Pastoral Theology).
- Fr. Beno Shao >Kutoka Nyumba ya malezi Morogoro na kwenda kwa utume Uaskofuni-Moshi.

**KIFO. Tukiwa katika kuandika WARAKA huu, tumepokea msiba wa kifo cha Mama Juliana Ragita mama wa Padre Peter Mwikwabe ambaye atafanyiwa mazishi tarehe 12.12.2023. Apumzike kwa amani-Amina.**

## 5. Malezi endelevu (On-going formation programme) ya Shirika

Yatafanyika mwaka ujao mwezi wa sita kwa Mapadre miaka saba rudi chini. Ratiba itatolewa muda ukifika.

## 6. Adhimisho la Jubilee ya miaka hamsini (50) ya Shirika, Novemba, 2024

Kwa uzinduzi uliofanyika sasa tupo kwenye maadhimisho haya ya mwaka wa Jubilee hadi kilele chake Novemba, 2024. Tujitahidi kutegemeza tukio hili lifanyike vema kwa ile michango tuliyokusudia.

Wanashirika kokote tulipo tuadhimishe kwa furaha tukio hili tukitafuta daima neema ya Mungu katika Utume wetu na msamaha kwa madhaifu yetu na wengine. Tujipatanishe na Mungu na tujipatanishe na wenzetu.

Matukio mbalimbali tuliyodhamiria kuyafanya na kuyaadhimisha muda huu yafanyike kwa uelewa wa kuwa kwenye utendaji bora wa kujali zaidi na kwa uadilifu.

## 7. JINA RASMI LA SHIRIKA

Hili tulitoa kwenye Waraka uliopita na tunalirudia tena kwa kusudi pekee tujifunze Jina la Shirika kwa usahihi wake kwani ndiyo Utambulisho (Identity) wa msingi wa Shirika.

**Kwa KIINGEREZA**

**The Apostolic Life Community of Priests in the Opus Spiritus Sancti (ALCP/OSS).**

**Kwa KISWAHILI**

**Mapadre wa SHIRIKA la Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu.**

**SHIRIKA la Mapadre wa Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu.**

**Mapadre wa JAMII ya Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu.**

**JAMII ya Mapadre wa Maisha ya Kitume wa Kazi ya Roho Mtakatifu.**

8. **Semina, Jubilee na Mafungo, 2024**

**KUNDI LA KWANZA tarehe 09.01.2024 hadi tarehe 20.01.2024 SABUKO**

**Jumanne, 09.01. 2024.......................................................... Kufika Sabuko.**
**Jumatano 10.01.2024......................................................... Jubilee.**
**Alhamisi na Ijumaa, 11.01.2024 na 12.01.2024.................... Semina.**
**Jumamosi na Jumapili, 13.01.2024 na 14.01.2024............... Mapumziko.**
**Jumapili jioni, 14.01.2024 hadi Ijumaa jioni, 19.01.2024.........Mafungo.**
**Jumamosi, 20.01.2024......................................................... Kuondoka.**

**SENDING CEREMONY >>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>> JUMATATU, 29.01.2024.**

**KUNDI LA PILI tarehe 31.01.2024 hadi tarehe 10.02.2024 SABUKO**

**Jumatano, 31.01.2024.......................................................... Kufika Sabuko.**
**Alhamisi na Ijumaa, 01.02.2024 na 02.02.2024...................... Semina.**
**Jumamosi na Jumapili, 03.02.2024 na 04.02.2024................. Mapumziko.**
**Jumapili jioni, 04.02.2024 hadi Ijumaa jioni, 09.02.2024..........Mafungo.**
**Jumamosi, 10.02.2024......................................................... Kuondoka.**

**Tupate majina ya wanaoshiriki KUNDI LA KWANZA na KUNDI LA PILI. Tukumbuke hili la kutuma MAJINA tafadhali.**

Wajubilee wetu mwaka huu ni;

i. **Padre Charles Lwanga Lyimo, ALCP/OSS.**
ii. **Padre Amedeus Ndeng'aso, ALCP/OSS.**
iii. **Padre Beda Msaki, ALCP/OSS.**
iv. **Padre Laurent Mtaroni, ALCP/OSS.**
v. **Padre Paul Materu, ALCP/OSS.**
vi. **Padre Theobald Weria, ALCP/OSS.**

**Tunawatakia nyote afya njema, NOELI NJEMA na MWAKA MPYA, 2024 wa baraka na MAADHIMISHO YA KUFANA YA MWAKA WA JUBILEE YA DHAHABU YA SHIRIKA.**

**Pd. Calistus Kirongozi.**
**Mkuu wa Shirika-Kanda, ALCP/OSS.**

ALCP/OSS PROVINCIAL OFFICE P.O. Box 724 MOSHI TANZANIA

**Pd. Jerome J. Okama.**
**Katibu.**